

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA HAMSINI NA TISA**

**04 JULAI, 2017**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA HAMSINI NA TISA – TAREHE 04 JULAI, 2017

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*].

### MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*].

### MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa

Mwaka 2017 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017].

### III. MASWALI:

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

#### 487. MHESHIMIWA MARWA RYOBA CHACHA (SERENGETI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wilaya ya Serengeti ni kitovu cha utalii na ni Wilaya inayopata watalii wengi lakini haina Hospitali ya Wilaya hivyo kuleta usumbufu kwa wageni pamoja na wakazi wa Serengeti:-

Je, ni lini Hospitali ya Wilaya itakamilika.

#### 488. MHESHIMIWA DKT. RAPHAEL MASUNGA CHEGENI (BUSEGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mji Mdogo wa Lamadi kwa muda mrefu umeidhinishwa kuwa Halmashauri ya Mji Mdogo:-

Je, ni lini sasa utekelezaji wake utaanza.



**489. MHESHIMIWA DOTO MASHAKA BITEKO (BUKOMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wilaya ya Bukombe ina mahitaji ya Walimu wa Shule za Msingi wapatao 1,425, waliopo ni 982 na upungufu ni 443:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Walimu wa kutosha kuondoa upungufu huo.

**WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

**490. MHESHIMIWA PETER AMBROSE LIJUALIKALI (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Serikali ilibinafsisha viwanda mbalimbali nchini ili kuongeza tija katika uzalishaji na kutengeneza ajira kwa Watanzania:-

(a) Je, Serikali ina mpango wowote wa kuvirudisha Serikalini viwanda vyake vilivyobinafsishwa kwa Wawekezaji na wakashindwa kuviendeleza hususan Viwanda vya MMT, NDC na UWOP vilivyopo Mang'ula/ Mwaya;

(b) Je, Serikali haioni kama kuendelea kuviacha Viwanda hivi kwa Wawekezaji walioshindwa

kuviendeleza na kuamua kukata mashine za Viwanda na kuuza kama chuma chakavu ni uhujumu wa Taifa.

**WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

**491. MHESHIMIWA HAWA ABDULRAHMAN GHASIA (MTWARA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha Wavuvi wa Mtwara Vijijini ili waweze kufanya uvuvi wa kisasa zaidi.

**492. MHESHIMIWA MASOUD ABDALLA SALIM (MTAMBILE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Wakulima wamezitumia vyema mvua kwa kulima mazao ya chakula na biashara lakini wanaendelea kupata hasara kubwa kwa kukosa masoko ya uhakika:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa ziada wa kuwapatia masoko ya uhakika Wakulima.

## **WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

### **493. MHESHIMIWA JOSEPHINE TABITHA CHAGULLA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Wanawake wengi wa Vijijini hawakopesheki kwa sababu Benki haziwafikii, pia hawana mafunzo maalum ya kuwasaidia ujuzi wa namna ya kufikia huduma hiyo ya kukopeshwa:-

- (a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa akina mama hao mafunzo maalum yatakayowasaida katika kujipanga kukopa;
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma ya Benki vijijini ili Wanawake wa huko waweze kupata mikopo.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **494. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Mara nyingi kumekuwa na taarifa juu ya watu wanaokamatwa na dawa za kulevya kwenye maeneo mbalimbali nchini lakini hatuambiwi nini kinafanyika:-

Je, baada ya watu hao kukamatwa ni nini huwa kinaendelea.



**495. MHESHIMIWA JUMA OTHMAN HIJA  
(TUMBATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kumekuwa na matukio yasiyo ya kawaida na kukaribia kuhatarisha amani katika Kisiwa cha Tumbatu:-

Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kujenga kituo cha Polisi katika Kisiwa hicho ili kukabiliana na matukio ya kihalifu.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**496. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL  
ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Pamoja na jitihada nyingi zinazofanyika, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imeendelea kuwa na tatizo la maji kila siku:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha na kukarabati Bwawa la Mindu ili kusaidia Wananchi wa Manispaa ya Morogoro kupata maji ya kutosha.

#### **IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na  
Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*].

**DODOMA  
04 JULAI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**

